JAMUHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
OFISI YA RAIS – TAMISEMI
HALMASHAURI YA MANISPAA ILEMELA

Kumb.Na.LSS /J.INSTR/VOLI/03

MZAZI/MLEZI WA MWANAFUZI
.....
SLP .....
.....

SHULE YA SEKONDARI BUSWELU
SLP 11164
MWANZA
Simu: 0717620103/ 0784821150
Email:buswelusecschool@gmail.com
ILEMELA- MWANZA.

YAH:MAAGIZO YA KUJIUNGA NA SHULE YA SEKONDARI BUSWELU-MWANZA KIDATO CHA TANO MWAKA 2021/2022:

Nafurahi kukujulisha kuwa mwanao amechaguliwa kujiunga Kidato cha **tano** kwa mwaka wa masomo **2021 /2022** katika shule hii, kwa **TAHASUSI YA.....**

Shule ya Sekondari Buswelu ni Shule ya Mchanganyiko ya Kutwa na ipo Umbali wa **Km 8** Kaskazini Mashariki mwa Jiji la Mwanza, Na **km 1.5 kutoka makao makuu ya** Manispaa ya Ilemela.

Tunakupongeza sana na tunakukaribisha hapa ujiunge na jumuiya nzima ya **BUSWELU SEKONDARI**. Hivyo ni mategemeo yetu kuwa utakuwa ni Mwanafunzi mwenye **kujitambua** mwenyewe na **Unayetambua** umuhimu **wa ELIMU**.

Aidha ni matarajio yetu kwamba utakitumia vizuri / vyema kipindi cha Miaka yako miwili **(2)** hapa Shuleni kwa **Bidii, Uaminifu, Uadilifu** na **Hekima** kubwa ili kulijenga Taifa letu.

Kama dhamira yako ni tofauti na Maelezo hapo juu, Unapaswa ubadilike ili Usitengeneze kizazi cha Wajinga katika Taifa letu. Taifa hili linajengwa nawe baada ya kupata **Elimu** bora itolewayo shuleni hapa.

" HONGERA NA KARIBU SANA"

Mahali shule ilipo

Shule ya sekondari Buswelu iko katika kata ya Buswelu, Manispaa ya Ilemela Mkoani Mwanza. Shule inafikika kiurahisi kwani kuna usafiri wa magari ya abiria (daladala) kutoka mjini hadi Buswelu. Magari hayo yanapatikana kwenye stendi iliyoko Mtaa wa Miti mirefu karibu na Hospitali ya Aghakhan. Panda magari yaliyoandikwa Buswelu/Ilalila – Mwanza au Buswelu/Isela – Mwanza ushukie kituo cha kona Bar.

Mwaka wa masomo utaanza tarehe 05.07.2021 na unatakiwa kuripoti shuleni tarehe **03.07.2021.** Tafadhali ripoti mapema tayari kwa kuanza masomo.
Mwisho wa kuripoti ni tarehe **31/07/2019** baada ya hapo nafasi itajazwa na wanafunzi wengine wenye uhitaji wa Elimu.

2.0. MAMBO MUHIMU YA KUZINGATIA:

2:1 Ujapo kuripoti shuleni hapa unapaswa kuja na;

a) Nakala kivuli (photocopy) ya Cheti cha kuzaliwa.
b) Fomu ya ukubali wa mwanafunzi kufuata sheria, taratibu na kanuni za shule Iliyojazwa kikamilifu.
c) Fomu ya mzazi kukubaliana na Sheria, taratibu na Maelekezo muhimu ya shule iliyojazwa kikamilifu.
d) Fomu ya Historia ya Mwanafunzi iliyojazwa kikamilifu.
e) **Fomu ya AFYA** yenye kuonesha vipimo vya magonjwa (Medical Examination form) iliyojazwa kikamilifu katika Hospital za Wilaya, Mkoa au Rufaa na **siyo Zahanati**.

2.2. SARE YA SHULE WASICHANA. (WASIOVAA HIJAB)

SARE YA SHULE

(a) Shati mbili nyeupe **polyster/tetron** zenye mikono mirefu ambazo hazibani mwili na ziwe na mfuko mmoja kushoto. Zinavaliwa kwa kuchomekea
(b) Sketi mbili ndefu sentimeta ishirini **(30 cm)** kutoka magotini. Rangi ya sketi ni **bluu bahari** Kitambaa cha Suti**. Mshono ni Boksi Marinda moja kubwa katikati mbele na nyuma na rinda za kawaida tatu kushoto na tatu kulia. (kitambaa na mshono imeambatanishwa)**
(c) Nguo za kushindia (Shamba dress) jozi mbili mbili rangi ya **Ugoro** kitambaa cha **SukariSukari**. Mshono ni Rinda Boksi kama ilivyo kwa Sketi. (Mshono na kitambaa imeambatanishwa).
(d). Viatu vya shule ni vyeusi vya ngozi vya kufunga na kamba vyenye visigino vifupi.
(g) Soksi jozi mbili nyeupe zinazofika chini ya goti na zisizo na pambo lolote.
(h) Tai rangi ya blue yenye kufanana na sketi yenye michirizi mieupe (pundamilia).

(i) Sweta moja rangi dark blue lenye michirizi miyeupe shingoni, mikononi na chini kiunoni.
(j) Sare za michezo ni **raba nyeupe** na track suit moja na jaketi lake rangi ya **bluu.**

2.3. SARE YA SHULE WASICHANA. (WANAOVAA HIJAB)

(a) Sketi mbili ndefu inayofika katika vifundo vya miguu na pana. Rangi ya sketi ni **bluu bahari** Kitambaa cha Suti**. Mshono ni Boksi Marinda moja kubwa katikati mbele na nyuma na rinda za kawaida tatu kushoto na tatu kulia.**
(b). Nusu kanzu inayofika chini ya makalio isiyofunika viganja vya mikono, iwe pana isibane.
(c). Kitambaa cha kichwani (ushungi), Kiwe kipana, Kiwe kirefu kisichofunika viganja vya mikono, Kisifunike uso na Kisiwe chepesi.
(d) Nguo za kushindia (Shamba dress) jozi mbili mbili rangi ya **Ugoro** kitambaa cha **SukariSukari**. Mshono ni Rinda Boksi kama ilivyo kwa Sketi. (Mshono na kitambaa imeambatanishwa).
(e). Viatu vya shule ni vyeusi vya ngozi vya kufunga na kamba vyenye visigino vifupi.
(f) Soksi jozi mbili nyeupe zinazofika chini ya goti na zisizo na pambo lolote.
(g) Sweta moja rangi dark blue lenye michirizi miyeupe shingoni, mikononi na chini kiunoni.
(h) Sare za michezo ni **raba nyeupe** na track suit moja na jaketi lake rangi ya **bluu.**

NB. **Masweta ya Rangi nyingine mbali na bluu pamoja na Majaketi hayatakiwi kabisa kuvaliwa shuleni hapa.**

2.4. ADA - ILIPWE BENKI YA NMB AKAUNTI YA SHULE NAMBA 31101200162.
Jina la Akaunti ni **BUSWELU SEC. SCHOOL RECURRENT**.

(a) Ada ya Shule kwa mwaka ni shilingi elfu sabini **(70,000/=)** kwa mwanafunzi wa bweni. Unaweza kulipa kiasi cha shilingi elfu thelathini na tano **(35,000/=)** kwa muhula au kulipa ada yote kwa mara moja. Fedha hizo zilipwe kwenye Akaunti ya Shule Na. **31101200162** katika Benki ya NMB tawi lolote. Jina la akaunti ni **BUSWELU SEC. SCHOOL RECURRENT.** (**Tafadhali, Tafadhali andika jina la mwanafunzi kwenye pay in slip).**

(b) MICHANGO MINGINE INAYOTAKIWA KULIPWA NA KILA MZAZI WA MWANAFUNZI WA BWENI ILIPWE BENKI YA NMB AKAUNTI NAMBA 31102515857. Jina la Akaunti ni BUSWELU SEC. SCHOOL E.K

(I) Shilingi elfu ishirini (20,000/=) kwa ajili ya ukarabati wa samani
(II) Shilingi elfu kumi (10,000/=) kwa ajili ya kitambulisho na Nembo
(III) Shilingi elfu thelathini (30,000/=) kwa ajili ya taaluma
(IV) Shilingi elfu Arobaini (40,000/=) kwa ajili ya malipo ya wapishi, walinzi na vibarua wengine
(V) Shilingi elfu kumi na tano (15,000/=) kwa ajili ya Huduma yakwanza
(VI) Shilingi elfu kumi (10,000/=) fedha ya tahadhari (haitarejeshwa)
(VII) Shilingi elfu thelathini na tano (35,000/=) kwa ajili ya maji na umeme.
(VIII) Bima ya Afya shilingi Elfu hamsini na mia nne (50,400/=) kwa mwanafunzi asiyekua na bima ya Afya. Kwa wanafunzi wenye bima ya Afya waje na vitambulisho Kila mwanafunzi ajiunge na mfuko wa **BIMA YA AFYA NHIF / CHF na aje na Kitambulisho cha Bima shuleni)**

ANGALIZO:

· Fedha za Michango hii zilipwe kwenye Akaunti ya Shule Na**. 31102515857** katika Benki ya **NMB** tawi lolote. (Jina la akaunti ni **BUSWELU SEC. SCHOOL E.K)**
ISICHANGANYWE NA PESA YA ADA

(C) MAHITAJI MUHIMU AMBAYO MWANAFUNZI WA BWENI ANAPASWA KULETA SHULENI

(I) Ream ya karatasi moja (01) Double "A"
(II) Godoro moja (01) futi 2.5 x 6
(III) Mashuka jozi mbili (02), jozi moja yenye rangi ya pink na foronya yake, na jozi nyingine rangi ya blue na foronya yake, chandarua moja (01) nyeupe
(IV) Scientific Calculator Kwa wanafunzi kwa wanafunzi wote.
(V) Dissecting kit kwa wanafunzi wa tahasusi ya PCB.
(VI) Dust cort moja (01) nyeupe kwa wanafunzi wote. **(Huvaliwa wakati wa practical tu).**
(VII) Vyombo vya chakula (sahani, bakuli, kijiko na kikombe)
(VIII) Vifaa vya usafi kimojawapo kati ya hivi. (Soft Broom 01, Hard Broom 01, Rubber Squizor 01)
(IX) Ndoo mbili ndogo za lita kumi zenye mifuniko kwa kila mwanafunzi kwa matumizi yake binafsi.
(IX) Vitabu vya masomo ya **TAHASUSI (COMBINATION)** Husika (Orodha imeambatanishwa)
(X) Mpatie mwanao fedha za matumizi za kutosha kadhalika mnunulie nguo za ndani za kutosha
(XI) Mnunulie sanduku la bati moja (trunker). Asije na begi / mabegi ya nguo za nyumbani.

MUHIMU
Unaweza kupata mahitaji haya kwenye maduka yaliyo karibu na shule ili kuepuka usumbufu wa mizigo mingi.

NA:	SOMO	JINA LA KITABU	JINA LA MWANDISHI
	PHYSICS	College Physics. Principles of physics.	Jerry D. Wilson S. Chands
	CHEMISTRY	Conceptual Chemistry (class xi). Conceptual Chemistry (class xii). General with Physical Chemistry. Advanced Level inorganic Chemistry Part I. Advanced Level Inorganic Chemisrty Part II.	Chand's Chand's APE
	ADVANCED MATHEMATICS	Advanced level pure maths Pure mathematics 1 & 2 Pure maths for class xii vol. 1 Pure maths for class xi Advanced maths Review Engineering Maths	C.J. Tranter J.K Back House, S.P.T. Houlds worth S. Chands s. Chands strout
	BASIC APPLIED MATHEMATICS (BAM)	Basic for Advanced Sec. school For form v and vi Basic for Advanced Sec. school For form v and vi	Septine Sillem TIE
	BIOLOGY	Understanding Biology Biological Science. Advanced Biology Third ED. Advanced Biology. Functional Approach .	SUZAN KIRA ROBERT KAROLA
	GEOGRAPHY	Phsical Geography of Africa with Diagrams Geography an intergrated Approach Practical Geography of East Africa	Burnett David Waugh Pritchad
	GENERAL STUDIES	General Studies for Advanced General Studies Supplementary book and Colleges Undestanding Advanced Level Sec. School Education Contemporary Approach for Advanced Level General Studies Notes	Richard Mbalase & Nyambari Nyangwine Civic EducationTeachers Association Nyambari Nyangwine

3. MAKOSA YATAKAYOSABABISHA MWANAFUNZI KUFUKUZWA SHULE

(i) Wizi
(ii) Kutohudhuria masomo kwa zaidi ya siku tisini (90) bila tarifa/utoro
(iii) Kugoma, kuchochea, kuongoza na kuunga mkono mgomo.
(iv) Kutoa lughja chafu kwa wanafunzi wenzake, walimu/ walezi na jamii kwa ujumla
(v) Kupigana mwanafunzi kwa mwanafunzi, kumpiga mwalimu au mtu yeyote Yule
(vi) Kusuka kuweka dawa kwenye nywele, **kunyoa kipara** au mitindo mingine kama `'**kiduku**''
(vii) Makosa ya jinai
(viii) Ulevi na matumizi ya pombe na madawa ya kulevya kama vile bangi, mirungi, kuberi, cocaine n.k
(ix). Kulala nje ya shule bila ruhusa.
(x). Kudharau Bendera ya Taifa/wimbo wa Taifa
(xi) Uasherati.
(xii) Ubakaji/ kusagana.
(xiii) Kuharibu kwa makusudi mali ya shule.
(xiv) Kuolewa.
(xv) Kuwa na **simu ya mkononi** shuleni.

3.1.SHERIA NA KANUNI MUHIMU ZA SHULE HII.

Shule inaendeshwa kwa mujibu wa sheria ya Elimu Na.25 ya mwaka 1978. Aidha imezingatia miongozo yote itolewayo na **wizara** yenye dhamana ya **Elimu** nchini. Unatakiwa kuzingatia mambo yafuatayo;-

I .Heshima kwa walimu, **viongozi**, **wazazi, wafanyakazi wasio walimu, wanafunzi wengine na jamii kwa ujumla**

II. Mahudhurio mazuri darasani na katika kila shughuli ifanyikayo ndani na nje ya shule..

III. Kuwahi katika shughuli zote za shule na zile utakazopangiwa.

IV. Kufahamu mipaka ya shule na kuzingatia kikamilifu maelekezo ya kuwepo ndani ya eneo la Shule wakati wote

VI.. Kutunza usafi wa mwili wako na mazingira ya shule.

VII. Kuvaa sare ya shule wakati wote unapotakiwa kufanya hivyo.

VIII. Kuzingatia ratiba ya shule wakati wote.

IX. Kofia, viatu vyenye urembo mapambo ya aina yoyote, **mikufu**, **bangili**, **heleni** haviruhusiwi na havitakiwi kabisa shuleni.

X. Kutunza **Mali ya Umma**.

XI. Kutotumia lugha mbaya wakati wowote kwa wanafunzi wenzake, walimu/wafanyakazi na kwa watu wengine.

XII. Kushirikiana na kusaidiana na wanafunzi wenzake katika kazi.

XIII. Kuthamini na kuheshimu kazi za aina zote.

XIV. Kuwa na kucha fupi zisizo pakwa rangi, na nywele fupi pia ziwekwe katika hali ya usafi kila wakati.

XV. kuvaa mavazi ya heshima.

XVI. Kuitika mara moja na kukimbia kuelekea aliko mtu anayekuhitaji (mwalimu/mfanyakazi/kiranja).

XVII. Kuheshimu ukumbi wa mikutano, ukumbi wa chakula, ofisi za shule, mali ya binafsi na mali ya umma.

XVIII. Kusimama katika mstari wakati wa kupokea huduma

XIX. Kuwa mfano mzuri kwa heshima na tabia njema mahali popote ulipo

XX. Kunyoosha mkono juu na asimame anapouliza au kujibu swali

XXI. Kukaa kimya wakati wote anapokuwa darasani, asitoke bila ruhusa ya Mwalimu au Kiongozi wa darasani.

XXII. Ni marufuku kwa mwanafunzi kuleta vifaa vya gharama shuleni kama redio, video, simu za mkononi n.k.

4.0. SHERIA ZA BWENI.

1. Kila mwanafunzi wa bweni anawajibika kusoma , kuelewa na kutekeleza kwa vitendo sheria na kanuni zote za bweni.
2. Hairuhusiwi wageni kukaribishwa ndani katika eneo la bweni bila ruhusa ya uongozi wa shule.
3. Kila mwanafunzi anawajibika kutunza na kuangalia mali ya shule iliyoko bwenini.
4. Hairuhusiwi kulia chakula bwenini isipokuwa wanafunzi wote watalia chakula katika holi la kulia chakula litakalokuwa limeandaliwa. Kwa wanafunzi wagonjwa watalia chakula katika chumba cha matroni.
5. Kila mwanafunzi anapasa kuhakikisha kuwa mazingira ya Bweni (nje na ndani) ni masafi wakati wote kwa kuondosha uchafu unaoondoka kwa urahisi bila kuelezwa kufanya hivyo.
6. Ni kosa kutoa taarifa ya uongo kwa uongozi wa shule kwa makusudi ili kupata haki isiyostahili.

7. Kila mwanafunzi anatakiwa kuvaa vazi la kushindia baada ya saa za masomo darasani na si vinginevyo.

8. Ni kosa kuchanganya vazi rasmi la shule na lisilo rasmi.
9. Mwanfunzi aliyepewa ruhusa ya kwenda nje ya Shule , atavaa sare ya Shule.
10. Mwanafunzi wa Bweni anaweza kulala nje ya shule kwa kibali cha Mkuu wa Shule tu, na anatakiwa kuripoti anaporudi.
11. Ruhusa zote za wanafunzi wa bweni lazima zianzie kwa Matroni.
12. Ni kosa kushawishi , kuanzisha au kushiriki mgomo wa aina yoyote ile.
13. Matusi ya kusemwa au kuandikwa na kupigana hairuhusuwi popote Shuleni , kila mmoja anapaswa kuonesha upendo kwa mwenzake.
14. Kila mwanafunzi wa Bweni anawajibika kuhudhuria kipindi cha maandalio (Preparation) bila kukosa katika vyumba vilivyotengwa kwa muda uliopangwa.
15. Ni marufuku kumiliki au kutumia simu ya mkononi ndani na nje ya Bweni.ukikamatwa adhabu ni kufukuzwa shule na si vinginevyo.
16. **VIFAA VYA UMEME HAVITAKIWI KABISA NDANI NA NJE YA BWENI**.

5:0 Baada ya kusoma kwa makini Sheria Taratibu na Kanuni, Utapaswa kujaza hati ya kukubali kufuata sheria,taratibu na kanuni zilizopo shuleni na uwasilishe shuleni utakaporipoti. Mambo mengine muhimu unayopaswa kukamilisha na kuwasilisha shuleni ni;

(a) Unatakiwa kujaza ‘’Medical Examination Form” ijazwe na Mganga mkuu wa hospitali ya Serikali Uiwasilishe kwa Mkuu wa Shule mara tu unaporipoti shuleni.
(b) Fomu ya maelezo Binafsi kuhusu historia ya Mwanafunzi na Mkataba wa Kutoshiriki katika Migomo,Fujo,na Makosa ya jinai.
(c) Fomu ya Mzazi/Mlezi kukiri,kukubaliana na Sheria Taratibu na Kanuni na kwamba atakuwa tayari kushirikiana na Shule katika kumwongoza mwanaye kufuata Sheria,Taratibu na Kanuni za Shule.

Tafadhari soma kwa makini maelezo/maagizo haya na kuyatekeleza kikamilifu.

KARIBU SANA KATIKA SHULE HII
MOTTO WA SHULE “EDUCATION IS WEALTH”

ARSEN B. PETER.
MKUU WA SHULE
0746476110 / 0717620103

MAVAZI KWA WASICHANA

SKETI NA SHORT KANZU





SHAMBA DRESS



SKIRT

APPENDIX "A"

JAMUHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

OFISI YA RAIS – TAMISEMI

HALMASHAURI YA MANISPAA ILEMELA

MKUU WA SHULE,

SHULE YA SEKONDARI BUSWELU,

S.L.P.11164

MWANZA

Ndg,

YAH. KUKUBALI KUFUATA UTARATIBU,SHERIA NA KANUNI ZA SHULE

Mimi.....
[majina matatu ya mwanafunzi]

Nimepokea barua yako ya masharti ya kujiunga na shule ya sekondari Buswelu-Kutwa

Naahidi **kutii taratibu,sheria na kanuni** zote za shule kama nilivyosoma na **kuwatii walimu na walezi wangu wengine shuleni.**

Nitafanya **kazi zote za darasani** ambazo zitaliletea **Taifa sifa nzuri, maendeleo** na heshima. Nitajitahidi katika masomo yangu na kushiriki kufanya mitihani yote ya ndani shuleni na ile ya nje kama vile mock na Taifa. **Sitakwepa mtihani wowote.**

Endapo nitatenda kinyume na barua hii **Bodi ya shule na uongozi wa shule** unichukulie hatua stahili kwa kufuata sheria zilizopo shuleni.

*****Nimesoma **taratibu,kanuni** na **sheria** za shule kwa makini na kuelewa.

Jina la mwanafunzi.....

Sahihi .....

APPENDIX "B"

JAMUHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

OFISI YA RAIS – TAMISEMI

HALMASHAURI YA MANISPAA ILEMELA

SHULE YA SEKONDARI BUSWELU

FOMU YA MZAZI/MLEZI KUKUBALIANA NA SHERIA TARATIBU KANUNI NA MAELEKEZO MUHIMU YA SHULE:

Mimi mzazi/mlezi wa ..... nimeongea na kumfafanulia mtoto wangu maelekezo ya barua hii ikiwa ni taratibu, kanuni na sheria za shule na ameelewa.

Naahidi kukubaliana na **Sheria,Taratibu na Kanuni** na **Maelekezo** yote muhimu yamhusuyo Mwanangu**. Aidha,**

i.Nitaitikia wito wowote pindi ninapohitajika Shuleni.

ii.Nitawajibika mara moja pindi kijana wangu akipata Mimba ama Kusababisha Mimba ndani na nje ya shule.

iii.Nitafuatilia kwa karibu Mahudhurio ya Kijana wangu Shuleni.

iv.Nitafuatilia Maendeleo ya Kitaaluma ya kijana wangu.

v.Nitahakikisha kuwa kijana wangu hajihusishi na migomo ya aina yote kipindi chote awapo Shuleni.

vi.Nitahakikisha kuwa kijana wangu hamiliki simu ya mkononi awapo Shuleni kinyume na hapo nikae naye nyumbani

Jina la mzazi/Mlezi.....

Sahihi.....

Namba ya simu.....

Tarehe .....

APPENDIX "C"

OFISI YA RAIS
TAWALA ZA MIKOA N A SERIKALI ZA MITAA
HALMASHAURI YA MANISPAA YA ILEMELA
SHULE YA SEKONDARI BUSWELU

FOMU YA TAARIFA MUHIMU ZA MWANAFUNZI

A: HISTORIA YA MWANAFUNZI

1.Jina la mwanafunzi.....

2.Shule ya msingi aliyotoka.....

3. Tareha ya kuzaliwa ____/_____/_____

4.Dini /dhehebu.....

5.Jina la baba.....

6.Kazi ya baba.....

7.Simu ya kazini ..... simu ya nyumbani.....

8.Jina la mama.....

9.Kazi ya mama.....

10. Simu ya kazini.....simu ya nyumbani.....

11.Anuani ya mzazi..... kijiji/mtaa ..... Kata .....

12.Lugha unayoweza kuongea .....

13.Kabila lako .....

Unaishi na Wazazi wako hapa jijini- Taja (Ninaishi /Siishi na Mzazi)

Iwapo huishi na Mzazi andika;

14.Jina la Mlezi .....

15.Uhusiano .....

16.Kazi aifanyayo Mlezi.....

17.Namba ya simu ya Mlezi.....

Habari zingine za Familia

Wewe ni Mtoto wa ngapi katika Familia?.....

JINA LA KAKA/DADA	UMRI	KAZI AIFANYAYO	MAHALI ANAPOISHI

Saini yako..... Tarehe.....

APPENDIX '"D"

THE UNITED REPUBLIC OF TANZANIA

PRESIDENT'S OFFICE – REGIONAL ADMINISTRATION AND LOCAL GOVERNMENT

BUSWELU SECONDARY SCHOOL

MEDICAL EXAMINATION FORM

(To be completed by a Medical Officer in respect of all Form ONE (FI) entrance)

PUPIL'S FULL NAME.....

AGE.....SEX.....

BLOOD COUNT(RED AND WHITE).....

URINALYSIS.....

SYPHILIS TEST.....

EYE TEST.....

CHEST.....

SPLEEN.....

ADDITIONAL INFORMATION

(Eg physical defect/impairment or chronic disease requiring special treatment/attention)

.....

.....

I certify that I have examined the above pupil and recommend that she/he is fit/unfit to pursue secondary education.

Signed.....

Designation.....

Date...../...../20..

(Delete which is inapplicable)